JIMBO KUU LA DAR ES SALAAM
S.L.P. 167 DAR ES SALAAM

**ARCHDIOCESE OF DAR ES SALAAM**

Sokoine Drive 40,
P.O. Box 167,
Dar es Salaam, TANZANIA

Tel: +255 22 2113223
Fax : +255 22 2125751
E-mail: nyumba@cats-net.co.tz
katibudsm@gmail.com

JKD/KJ/XXV/COR/96

08 Agosti 2025

Waheshimiwa Madekano,
Maparoko,
Mapadri,
Watawa na Waamini Walei,
Jimbo Kuu la Dar es Salaam

Tumsifu Yesu Kristo,

**Yah: Maelekezo ya Askofu Mkuu wa Dar es Salaam Kuhusu Novena ya Kuliombea Taifa letu Haki na Amani**

Kwa barua hii, Madekano, Maparoko, Watawa na Waamini wote Walei wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam mnakumbushwa agizo ambalo Askofu wetu Mkuu Mhashamu Sana Jude Thaddaeus Ruwa'ichi OFMCap alilitoa siku ya tarehe 07.07.2025 katika Sherehe za Upadrisho katika Viwanja vya Msimbazi Center, kuhusu utaratibu wa Novena ya kuliombea Taifa letu Haki na Amani.

Mhashamu Sana Askofu Mkuu ameagiza kwamba katika Parokia zote na Asasi zote katika Jimbo Kuu la Dar es Salaam ifanyike Novena ya siku tisa **(9)** kuomba Haki na Amani kuanzia tarehe **15 – 23 Agosti 2025**. Askofu Mkuu ameelekeza kwamba Novena hiyo iambatane na kuabudu Ekaristi Takatifu, Kusali Rozari Takatifu na kusali sala ya Kuiombea Tanzania kama iliyotolewa na Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC).

Aidha, katika siku ya kilele cha Novena hiyo, yaani Jumamosi tarehe **23 Agosti 2025**, ambayo kwa Kanisa zima la Tanzania ndiyo siku ya **kufunga na kukesha katika kusali** kwa ajili ya kuomba Haki na Amani, sote tunaalikwa kufuata Ratiba iliyotolewa na Idara ya Kichungaji ya Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) ambayo inaelezea namna ya kufanya sala na mfungo huo ambao utaanza hiyo tarehe 23 Agosti kwa adhimisho la Ekaristi Takatifu, ikifuatiwa na kuabudu Ekaristi Takatifu ikiambatana na vipindi mbalimbali vya sala, mafundisho, na ukimya, na kuhitimishwa Dominika tarehe 24 Agosti kwa adhimisho la Misa Takatifu kama inavyoelekezwa katika maelekezo yaliyotoka TEC. Hapa inapendekezwa kwamba katika Parokia zote Misa hii ya hitimisho la kesha iwe Misa ya kwanza.

**Nyongeza:** Sala mbalimbali ambazo zimeelekezwa/ zimependekezwa katika Ratiba hii iliyotolewa na TEC tunaweza pia kuzitumia katika kusali Novena iliyoelekezwa hapo juu.

Barua ya TEC na mwongozo na sala vimeambatishwa hapa chini.

Tunawatakieni utekelezaji mwema wa maadhimisho hayo.

Pd. Vincent Mpwaji
*Chancellor* – Jimbo Kuu la Dar es Salaam

ARCHDIOCESE OF DAR ES SALAAM
CHANCELLOR
P. O. Box 167
Tel: 022 2113223
DAR-ES-SALAAM . TANZANIA

## SALA YA KUIOMBEA TANZANIA

Ee Mungu Mwenyezi wa milele, Baba wa mataifa yote na wa watu wote, utuangalie kwa macho ya huruma sisi watu wako wa Tanzania, ambao nasi sasa twahesabika kati ya mataifa ya dunia. Kwa baraka yako uhuru wetu huu usipokonywe, na utuwezeshe kuishi maisha mema zaidi kadiri iwastahilivyo waana wa Mungu.

Tunakuomba nchi yetu iwe ya amani, waliopotea wapatikane na waliotekwa wapate uhuru wao, walioumizwa wapone, na waliouawa wapate uzima wa milele na uovu ukome katika nchi yetu. Tunakuomba ubadilishe nyoyo za watenda maovu na washirika wao katika uovu ili zikuelekee wewe, kwani sisi tulio wanyonge hatuna uwezo wa kuzibadilisha nyoyo ovu.

Uendelee kututawala na kutuongoza. Daima nchi hii iongozwe na viongozi ambao ni chaguo lako. Waangazie watawala hao, sheria wanazotunga kwa kutufaidia kwa mambo mema ya hapa duniani zipatane na Wewe uliyetuumba kwa ajili yako. Wajalie watu wetu wote paji lako la Imani. Tukiwa Mahujaji wa Matumaini, tuthibitishe tusishindwe kupambana na maovu yawezayo kutufikia kutoka nje au ndani, tupe hekima ya kutafuta ukweli katika mambo yote, na kuishi kwa uaminifu katika amri zako.

Ee Mwenyezi Mungu, uongozi wa kweli unatoka kwako, tunakuomba ujalie wale watakaosimamia na kuiishi Demokrasia ya kweli, Haki na Amani katika nchi yetu ili haki ituletee Amani ya kudumu.

Washa nyoyo zetu na mapendo yako ya kimungu yatakayotuwezesha kushinda utengano, ushindani, na chuki ya ukabila au utaifa, na tuunganishe wote katika muungano wa kidugu utakaotuwezesha, kwa msaada wa neema yako, kutufanya tuwe umoja katika Wewe Baba wa wote.

Tunaomba hayo kwa njia ya Kristo Bwana wetu. Amina.

**Bikira Maria Mtakatifu Mkingiwa dhambi ya asili. Utuombee.**

**Atukuzwe Baba....**

CATHOLIC SECRETARIAT

TANZANIA EPISCOPAL CONFERENCE

P.O BOX 2133
PHONE 022/2851075-7-8
022/2850047
022/2850017
FAX 022/2851133; 2850427
DOMAIN: TEC.CO.TZ
E-Mail: info@tec.or.tz
DAR ES SALAAM
TANZANIA

***Department: PASTORAL***

***Reference: TEC/P/05/08/25*** ***05/08/2025***

**YAH: RATIBA YA MFUNGO KUOMBA HAKI NA AMANI NCHINI TAREHE 23 AGOSTI 2025**

Wapendwa Kristo ni Tumaini Letu.

Naomba turejee Barua ya Maaskofu ya tarehe 19 Juni 2025 iliyotoa mwito wa kuwa na siku ya Sala na Mfungo kuombea Haki, Usawa, Ukweli, Mshikamano na Ustawi wa wote ambavyo tunda lake ni Amani. Pamoja na utaratibu ambao kila Jimbo litajipangia katika kutekeleza wito huo, tunaomba mpokee mapendekezo yafuatayo yatakayotumika kama Mwongozo wa jinsi ya kuiadhimisha siku hii maalum kwa Sala na Mfungo.

**SAA: 2:00 – 03:00 Asubuhi**

**Misa Takatifu ya Ufunguzi: KWA AJILI YA KUDUMISHA AMANI NA HAKI**
*Misa na. 30 (rej. Misale ya Kiroma uk, 931-932).* ***(Angalia kiambatanisho mwishoni mwa barua hii)***

**Kuabudu Ekaristi Takatifu**
Lengo: kuabudu, kuikabidhi nchi yetu ya Tanzania Kwa Mungu

**SAA: 3:00 – 5:00 Asubuhi**

Waongozaji: MAKATEKISTA NA WATUMIKIZI
Mafundisho ya Biblia
Kipindi cha kimya binafsi mbele ya Ekaristi Takatifu na Maungamo

**SAA: 5:00 – 7:00 Mchana**

Waongozaji: UTOTO MTAKATIFU NA WALEZI WAO – Kuabudu kwa Watoto
Mafundisho: Yesu rafiki wa watoto
Sala Ya Kuombea haki na amani nchi yetu na nyimbo
Kipindi cha kimya binafsi mbele ya Ekaristi Takatifu na Maungamo

**SAA: 7:00 – 9:00 Mchana**

Waongozaji: KWAYA
Sala ya Malaika wa Bwana na Rozari Ya Huruma ya Mungu
Nyimbo za kusifu na kuabudu Ekaristi Takatifu
Kipindi cha kimya binafsi mbele ya Ekaristi Takatifu na Maungamo

**SAA: 9:00 Alasiri – 11:00 Jioni**

Waongozaji: VIJANA
Neno la Mungu na Litania ya Bikira Maria
Kipindi cha kimya binafsi mbele ya Ekaristi Takatifu na Maungamo

**SAA: 11:00 – 12:00 Jioni**

Waongozaji: UWAKA
Tafakari ya Neno la Mungu
Kipindi cha kimya binafsi mbele ya Ekaristi Takatifu na Maungamo
Litania ya Moyo Mt. wa Yesu

**SAA: 12:00 – 2:00 Usiku**

Waongozaji: WAWATA
Rozari Takatifu na Litania ya Bikira Maria
Ukimya na Maungamo

**SAA: 2:00 – 4:00 Usiku**

Waongozaji: WATAWA NA WASEMINARI NA MAPADRE
Mafundisho juu ya Huruma ya Mungu
Litania ya huruma ya Mungu
Tafakari ya mateso ya Kristo
Kipindi cha kimya binafsi mbele ya Ekaristi Takatifu

**SAA: 4:00 – 6:00 Usiku**

Waongozaji: JUMUIYA NDOGO NDOGO (JNNK)/KANDA KUNDI LA I
Ukimya na Sala za Kibinafsi
Nyimbo za Kusifu na kuabudu Ekaristi Takatifu
Maombi binafsi

**SAA: 6:00 – 8:00 Usiku**

Waongozaji: JUMUIYA NDOGO NDOGO (JNNK)/KANDA KUNDI LA II
Neno la Mungu na Litania ya Bikira Maria
Litania ya Jina Takatifu la Yesu
Kipindi cha kimya binafsi mbele ya Ekaristi Takatifu

**SAA: 8:00 – 10:00 Usiku**

Waongozaji: **MOYO MTAKATIFU WA YESU NA KARISMATIKI KATOLIKI**
Ukimya na Kuimba Nyimbo za Ekaristi Takatifu
Neno la Mungu na Litania ya Huruma ya Mungu
Kipindi cha kimya binafsi mbele ya Ekaristi Takatifu

**SAA: 10:00 – 12:00 Asubuhi**

Waongozaji: JUMUIYA NDOGO NDOGO (JNNK)/KANDA KUNDI LA III
Neno la Mungu
Kipindi cha kimya binafsi mbele ya Ekaristi Takatifu
Rozari Takatifu na Litania ya Bikira Maria
Sala ya asubuhi na Maandalizi ya Misa

**SAA: 1:30 – 3:30 Asubuhi**

MISA TAKATIFU YA KUFUNGA

**MAELEKEZO YA JUMLA**

- Kila kundi lishiriki kwa ukamilifu kulingana na muda wao.
- Sala ziwe na utulivu, heshima, na uchaji.
- Matumizi ya Biblia yawekwe kwa tafakari binafsi na ya pamoja.
- Kuhakikisha Ekaristi Takatifu haibaki peke yake kila saa.
- Siku ya kuhitimisha itaadhimishwa Misa ya Dominika lakini iwekwe nia ya kumshukuru Mungu kwa siku ya hii ya Mfungo na Sala.

**Niwatakie utekelezaji mwema wa maadhimisho haya matakatifu katika kuombea Haki na Amani**

......................................
Pd. Alister Makubi
**MKURUGENZI WA UCHUNGAJI-TEC**

TANZANIA EPISCOPAL CONFERENCE
PASTORAL DEPARTMENT
P.O. Box 2133
D'SALAAM

## <u>MISA NA. 30 (*Rej. Misale Ya Kiroma Uk, 931-932*).</u>

### 30. KWA AJILI YA KUDUMISHA AMANI NA HAKI

A

### Antifona ya kuingia

Ee Bwana, uwape amani wakungojao na usikilize sala za watumishi wako, ukatuongoze kwenye njia ya haki.

Taz. YbS 36:15-16 (neo Vulg)

### Kolekta

**Ee Mungu, umefunua kwamba wapatanishi wataitwa wana wa Mungu. Tunakuomba utujalie tuiimarishe bila kukoma haki ile ambayo peke yake inaleta kwa uhakika amani ya kudumu na ya kweli.**
**Kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo Mwanao, anayeishi na kutawala**
**nawe katika umoja wa Roho Mtakatifu, Mungu, milele na milele.**

### Au:

**Ee Mungu Baba, unawashughulikia watu wote kwa wema.**
**Uwe radhi kuwajalia wanadamu uliowapa chimbuko moja**
**wawe familia moja yenye amani,**
**na waunganishwe daima kwa roho ya udugu.**
**Kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo Mwanao, anayeishi na kutawala**
**nawe katika umoja wa Roho Mtakatifu, Mungu, milele na milele.**

*Sala nyingine zipo kwenye uk. 932.*

### Sala ya kuombea dhabihu

**Ee Bwana, sadaka ya Mwanao, Mfalme wa amani, iletayo wokovu,**
**ambayo inatolewa kwa ishara hizi za sakramenti**
**zinazoonyesha amani na umoja,**
**ifae kwa kazi ya kuimarisha uelewano kati ya wana wako wote.**
**Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**

**Itumike Sala ya Ekaristi ya Pili ya "Upatanisho" na Utangulizi wake (*Rej. Misale Ya Kiroma – Nyongeza kwenye Kanuni ya Misa Uk, 503 - 506*)**

**SALA YA EKARISTI YA PILI "YA UPATANISHO"**

K/. **Bwana awe nanyi.**
W/. **Na awe rohoni mwako.**
K/. **Inueni mioyo.**
W/. **Tumeiinua kwa Bwana.**
K/. **Tumshukuru Bwana Mungu wetu.**
W/. **Ni vema na haki.**

**Kweli ni vema na haki**
**tukushukuru na kukusifu wewe,**
**Ee Mungu, Baba mwenyezi,**
**kwa yote unayoyatenda katika ulimwengu huu,**
**kwa njia ya Yesu Kristo Bwana wetu.**

**Maana, japo familia ya wanadamu**
**imefarakana na kutengana kwa fitina,**
**tumefahamu na kutambua**
**kwamba wewe unaweza kulegeza mioyo,**
**ili watu wawe tayari kupatanishwa.**

**Maana, kwa njia ya Roho wako unaishawishi mioyo ya watu,**
**ili maadui warejee kwenye mazungumzano,**
**wapiganao wapeane mikono,**
**na mataifa watafute njia ya kukutana kwa amani.**

**Kwa uwezo wako tendaji , ee Bwana,**
**chuki ishindwe na upendo, kisasi kiuachie nafasi msamaha,**
**na ugomvi ugeuzwe kuwa urafiki.**

**Kwa sababu hiyo, sisi, pamoja na umati wa mbinguni,**
**tunakushukuru wewe daima**
**na kuisifu bila mwisho hapa duniani adhama yako kwa sauti kuu::**

W/. **Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu,**
**Bwana Mungu wa majeshi.**
**Mbingu na dunia zimejaa utukufu wako.**
**Hosana juu mbinguni.**
**Mbarikiwa ajaye kwa jina la Bwana.**
**Hosana juu mbinguni.**

Kuhani, hali amefumbua mikono, anasema:

**Kwa hiyo, ee Baba mwenyezi,** KK
**tunakuhimidi kwa ajili ya Yesu Kristo Mwanao,**
**aliyekuja kwa jina lako.**
**Yeye ndiye Neno awaleteaye wokovu wanadamu,**
**mkono unaowakaribisha wakosefu,**
**njia inayotuletea amani yako.**
**Wakati sisi tulipojitenga mbali nawe**
**kwa sababu ya dhambi zetu,**
**wewe, ee Bwana, ulituredisha kwenye upatanisho,**
**ili kwa kukuongokea wewe, sisi nasi tupate kupendana,**
**kwa njia ya Mwanao, uliyemtoa afe kwa ajili yetu.**

Anafumba mikono, na kuitandaza juu ya mkate na divai, akisema:

**Na sasa, tunapoadhimisha upatanisho**
**tulioletewa na Kristo,**
**tunakusihi:**
**uvitakatifuze vipaji hivi kwa kuvishushia Roho wako,**

anafumba mikono na kuandika ishara ya msalaba mara moja tu juu ya mkate na kalisi, akisema:

**ili viwe Mwili na + Damu ya Mwanao,**
**ambaye tunatimiza amri yake**
**kwa kuadhimisha mafumbo haya.**
Anafumba mikono.

Katika fomula zinazofuata, maneno ya Bwana yatamkwe kwa sauti bayana na dhahiri, inavyotakiwa na maumbile ya maneno hayo yenyewe.

**Maana, Yeye mwenyewe, alipokaribia kutoa uhai wake,** KW
**ili atukomboe sisi,**
**akiwa mezani**

anatwaa mkate, na kwa kuuinua kidogo juu ya altare, anaendelea kutamka:

**alitwaa mkate mikononi mwake,**
**na akikushukuru, aliubariki,**
**akaumega, akawapa wafuasi wake, akisema:**

anainama kidogo tu:

**TWAENI, MLE NYOTE:**
**HUU NDIO MWILI WANGU,**
**UTAKAOTOLEWA KWA AJILI YENU.**
Anawaonyesha waamini hostia takatifu, na kuiweka kwenye patena, na, akipiga goti, anaabudu.

Halafu anaendelea akisema:

**Vivyo hivyo, jioni ileile,**

anatwaa kalisi, na kwa kuuinua kidogo juu ya altare, anaendelea kutamka:

**alitwaa kikombe cha baraka mikononi mwake,**
**na, akikushukuru tena kwa rehema yako,**
**akawapa wafuasi wake, akisema:**
anainama kidogo tu:

**TWAENI, MNYWE NYOTE:**
**HIKI NDICHO KIKOMBE CHA DAMU YANGU,**
**DAMU YA AGANO JIPYA NA LA MILELE,**
**ITAKAYOMWAGIKA KWA AJILI YENU**
**NA KWA AJILI YA WENGI**
**KWA MAONDOLEO YA DHAMBI.**
**FANYENI HIVI KWA UKUMBUSHO WANGU.**
Anawaonyesha waamini kalisi, anaiweka juu ya korporale, na akipiga goti anaabudu.

Halafu anasema:
**Fumbo la imani.** **KK**

Na waamini wanaitikia:
**Ee Bwana, tunatangaza kifo chako,**
**na kutukuza ufufuko wako, mpaka utakapokuja.**

Au:
**Ee Bwana, kila tunapokula mkate huu**
**na kukinywea kikombe hiki,**
**tunatangaza kifo chako, mpaka utakapokuja.**

Au:
**Ee Mwokozi wa ulimwengu, utuokoe,**
**wewe uliyetukomboa kwa msalaba na ufufuko wako.**

Halafu, hali amefumbua mikono, kuhani anasema:
**Kwa hiyo, tunapoadhimisha ukumbusho** **KW**
**wa kifo na ufufuko wa Mwanao,**
**tunakutolea sadaka ya upatanisho kamili,**
**aliyotuachia kama amana ya upendo wake,**
**na ambayo wewe mwenyewe ulitukirimia.**

**Ee Baba uliye mtakatifu, tunakusihi kwa unyenyekevu,**
**utupokee sisi pia pamoja na Mwanao**
**na katika karamu hii iletayo wokovu**
**ukubali kutujalia Roho wake,**
**ili ayaondoe yote yanayotutenganisha sisi kwa sisi.**

**Yeye alifanye Kanisa lako liwe ishara ya umoja** **K1**
**na chombo cha amani yako kati ya watu wote,**
**na kutudumisha sisi katika ushirika**
**pamoja na Baba mtakatifu wetu J. na Askofu wetu J.***
**na Maaskofu wote na taifa lako lote.**

**Kama vile ulivyotukusanya sasa kwenye meza ya Mwanao, K2**
**hali kadhalika utukusanye pamoja na Bikira Maria,**
**Mama mtukufu wa Mungu,**

**na mtakatifu Yosefu, mume wake huyo Bikira,**
**Mitume wenye heri na Watakatifu wote,**
**pamoja na ndugu zetu,**
**na wanadamu wa kila kabila na lugha**
**waliofariki wakiwa na urafiki nawe.**
**Utujalie tujumuike nao kwenye karamu ya umoja wa milele,**
**katika mbingu mpya na dunia mpya,**
**unakoangaza utimilifu wa amani yako,**
anafumba mikono:
**katika Kristo Yesu Bwana wetu.**

Anatwaa patena yenye hostia takatifu na kalisi, na akiviinua vyote viwili, anasema:
**Kwa njia yake, na pamoja naye na ndani yake,**
**wewe, Mungu Baba mwenyezi,**
**katika umoja wa Roho Mtakatifu,**
**unapata heshima yote na utukufu**
**milele na milele.**

Na waamini wanashangilia:
**Amina.**

## Antifona ya Komunyo

Mt 5:9

Heri wapatanishi, maana hao wataitwa wana wa Mungu.

Yn 14:27

Au:

Amani nawaachieni, amani yangu nawapa, asema Bwana.

## Sala baada ya Komunyo

**Ee Bwana, tunakuomba utujalie roho ya mapendo,**
**ili, tukiwa tumetiwa nguvu kwa Mwili na Damu ya Mwanao pekee,**
**tustawishe kwa ufanisi kati ya wote**
**ile amani ambayo wewe mwenyewe umetuachia.**
**Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.**